



NAJIVUNIA KUWA MWEUSI

I AM PROUD TO BE BLACK



MTOTO MWEUSI

Mimi ni mtoto mweusi.

Mimi ni mwanafunzi.

Mimi nina vipaji vingi.

Nikiwa mkubwa naweza kufanya vitu vingi.



BLACK CHILD

I am a black child.

I am a student.

I have many talents.


When I grow up I can do many things.

VIONGOZI WEUSI

Kuna viongozi wengi weusi.

Viongozi kama Kamala na Mandela.

Nikiwa mkubwa, naweza kuwa kiongozi.



BLACK LEADERS

There are many Black leaders.

Leaders like Kamala and Mandela.


When I grow up I can become a leader.

WAVUMBUZI WEUSI

Kuna wavumbuzi wengi weusi.

Garret Morgan alivumbua taa za barabarani.

Nikiwa mkubwa naweza kuwa mvumbuzi.



BLACK INVENTORS

There are many Black Inventors.

Garret Morgan invented traffic lights.


When I grow up I can become an inventor.

WANAMICHEZO WEUSI

Kuna wanamichezo wengi weusi.

Wanamichezo kama Serena Williams na Michael Jordan.

Nikiwa mkubwa naweza kuwa mwanamichezo.



BLACK ATHLETES

There are many Black athletes.

Athletes like Serena Williams and Michael Jordan.

When I grow up I can become an athlete.

WAANDISHI WEUSI

Kuna waandishi wengi weusi.

Waandishi kama Marley Dias na Trevor Noah.

Nikiwa mkubwa naweza kuwa mwandishi.



BLACK AUTHORS

There are many Black authors

Authors like Marley Dias and Trevor Noah.

When I grow up I can become an author

WATETEZI HAKI WEUSI

Kuna watetezi haki wengi weusi.

**Watetezi kama Martin Luther King na
Harriet Tubman.**

Nikiwa mkubwa nitatetea haki za watu.



BLACK ACTIVISTS

There are many Black activists.

Activists like Martin Luther King and Harriet Tubman.

When I grow up I will advocate for peoples rights.

WASHAIRI WEUSI

Kuna washairi wengi weusi.

**Washairi kama Maya Angelou na
Amanda Gordon.**

Nikiwa mkubwa naweza kuwa mshairi



BLACK POETS

There are many Black Poets.

Poets like Maya Angelou and Amanda Gordon.


When I grow up I can become a poet.

WANASAYANSI WEUSI

Kuna wanasayansi wengi weusi.

Wanasayansi kama Mae Jemison na Katherine Johnson.

Nikiwa mkubwa naweza kuwa mwanasayansi.



BLACK SCIENTISTS

There are many Black Scientists.

Scientists like Mae Jemison and Katherine Johnson.

When I grow up I can become a Scientist.

WAIGIZAJI WEUSI

Kuna waigizaji wengi weusi.

Waigizaji kama Lupita Nyong'o and Denzel Washington.

Nikiwa mkubwa naweza kuwa mwigizaji.



BLACK ACTORS

There are many Black actors.

Actors like Lupita Nyong'o and Denzel Washington.

When I grow up I can become an actor.

MADAKTARI WEUSI

Kuna madaktari wengi weusi.

Madaktari kama Ben Carson na Rebecca Crumpler.

Nikiwa mkubwa naweza kuwa daktari.



BLACK DOCTORS

There are many Black Doctors.

Doctors like Ben Carson and Rebecca Crumpler.

When I grow up I can become a doctor.

WATAALAMU WESUSI

Duniani kote kuna wataalamu wengi weusi.

Wataalamu wa siasa, uchumi na biashara.

Wataalamu wa afya, elimu na mazingira.

Nikiwa mkubwa naweza kuwa mtaalamu
wa kitu chochote.

Weusi wangu ni fahari yangu.

Tujivunie kuwa weusi!



BLACK EXPERTS

Around the world there are many Black experts.

Political, economic and business experts.

Health, education and environmental experts.

When I grow up I can become an expert of anything.

My Blackness is my pride.

Let's be proud to be Black!

TUSHEREHEKEE WATU WEUSI

Watu weusi wana uwezo sawa na wengine.

Watu weusi wana haki sawa na wengine.

Rangi ya ngozi sio kipimo cha uwezo.

Tuache ubaguzi wa rangi.

Tusherehekee michango ya watu weusi.



LET'S CELEBRATE BLACK PEOPLE

Black people have equal ability like others.

Black people have equal rights like others.

Skin colour is not a measure of ability.

Let's stop anti-Black racism.

Let's celebrate Black People's contributions.

ZOEZI

Chagua jibu sahihi – Pick the right answer

1. Nani aligundua taa za barabarani?

- a. Nelson Mandela
- b. Garret Morgan
- c. Ben Carson

2. Nani ni mtetezi haki?

- a. Mae Jemison
- b. Serena Williams
- c. Martin Luther King

3. Lupita Nyong'o ni nani?

- a. Mshairi
- b. Mwanamichezo
- c. Mwigizaji

Watoto Mini Book Series by.....



To get more free & fun Swahili Learning resources visit

<https://www.swahilikids.com/>



@kiswahiliKIDS



@swahiliKIDS



@swahili.KIDS